

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA OFISI YA MKUU WA MKOA MTWARA

Taarifa kwa Umma



Jana Agosti 18, 2017 Chemba ya Wafanya biashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) wamezindua Meli ya Biashara itakayokuwa ikifanya safari zake kati ya Mtwara, Tanzania na Moroni, Comoro.

Kwa kuanzia, Meli iitwayo 'VILLE DE FOMBONI MOH 0022' itakuwa ikitia nanga Bandari ndogo ya Mtwara iliyoko karibu na Hoteli ya Southern Cross zamani ikiitwa Msemo Hotel.

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mtwara inawapongeza TCCIA kwa kufanikisha suala hili. Ujio wa meli hii ni hatua moja kubwa inayoashiria kufungua milango ya fursa za kibishara kati ya Mtwara, (Tanzania) na Moroni (Comoro). Wafanya bishara na wananchi wote wa Mkoa wa Mtwara wanatakiwa kuichangamkia fursa hii ili kukuza kipato cha mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla

Imeandaliwa na

Evaristy Masuha
Afisa Habari

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mtwara